Australian Government

my medicare

# Kutambulisha MyMedicare

Taarifa kwa wagonjwa



## Nini maana ya MyMedicare?

MyMedicare ni mfumo wa usajili wa wagonjwa wa hiari ambao unalenga kurasimisha uhusiano kati ya wagonjwa, daktari wako wa magonjwa ya jumla, daktari wa familia (GP) na timu za huduma ya msingi.

Kuonana na daktari wa familia wako mara kwa mara na kurasimisha uhusiano ulio nao na daktari wa familia wako na daktari wako wa magonjwa ya jumla a kupitia MyMedicare kunaweza kusababisha matokeo bora ya kiafya.

Kwa kujiandikisha kama mgonjwa na daktari wako wa magonjwa ya jumla  uliyochagua na kuchagua daktari wa famalia unayependelea, ufadhili wa ziada utapatikana kutoka kwa serikali ili kusaidia timu yako ya utunzaji wa msingi kutoa utunzaji unaohitaji.

Ni kwa hiari na bila malipo kujiandikisha katika MyMedicare, na usajili uko wazi kwa Waaustralia wenye kadi ya Medicare au Kadi ya Wazee (Veterani) ya Idara ya Mambo ya Wazee (DVA). Ili kujua kama unastahiki MyMedicare soma Usajili katika karatasi ya ukweli ya MyMedicare.

MyMedicare ni mfumo wa usajili na hautakuwa na taarifa zozote za afya yako. Maelezo yako ya afya ya kimatibabu yataendelea kuhifadhiwa katika Rekodi yako ya Afya Yangu (My Health Record), ikiwa unayo. Taarifa zote za kibinafsi zilizorekodiwa katika MyMedicare, ikiwa ni pamoja na watoa huduma wa afya uliowachagua, zitawekwa salama na faragha yako itadumishwa. Soma Notisi ya Faragha ya MyMedicare katika health.gov.au/mymedicare-privacy kwa maelezo zaidi.

Changanua msimbo huu wa QR kwa maelezo ya usajili

**Zungumza na daktari wako wa magojwa ya jumla (GP) au daktari kuhusu kujiandikisha katika MyMedicare, au upate maelezo zaidi kwenye health.gov.au/mymedicare**

my medicare

## Faida za kujiandikisha kwa MyMedicare

Maeneo mengi ya Matibabu ya magonjwa ya jumla kote Australia yamejiandikisha katika MyMedicare ili kuwasaidia katika kutoa utunzaji na huduma zinazolingana na mahitaji ya wagonjwa wao wa kawaida.

### Kwa kujiandikisha katika MyMedicare, unaweza kufaidika na:

**Uhusiano rasmi** na daktari wako wa magonjwa ya jumla au GP (daktari wa familia), ambao wameonyesha kuboresha matokeo ya afya.

**Faida za Mpango wa Medicare (MBS)** za mda mrefu zinayofadhiliwa na daktari wako wa afya.

**Motisha kwa mashauriano ya muda mrefu ya afya** kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka 16 na wenye Kadi ya Punguzo ya Jumuiya ya Madola, kuanzia tarehe 1 Novemba 2023.


**Kutembelea zaidi** daktari wako wa familia (GP) na kupanga utunzaji bora kwa watu wanaoishi katika makao ya kulea wazee, kuanzia Agosti 2024.

**Kuunganishwa kwa utunzaji unaofaa zaidi** ikwenye matibabu ya jumla kwa watu wanaotembelea hospitali mara kwa mara, kuanzia katikati ya 2024.

Mashauriano ya afya ya kwenye simu yanayofadhiliwa ya muda mrefu zaidi yanaweza kuwa ya manufaa kwa watu wanaotafuta usaidizi wa afya zao za akili, watu wenye ulemavu, Waaustralia wazee na watu wa vijijini au maeneo ya mbali ya Australia.

Manufaa zaidi ya usajili kwa wagonjwa yataendelea kuongezwa kama sehemu ya dhamira ya Serikali ya Australia katika kuimarisha Medicare. Ukichagua kutojisajili katika MyMedicare, bado utaweza kufikia ubora sawa wa huduma kutoka kwa watoa huduma wako wa afya.







Changanua msimbo huu wa QR kwa maelezo ya usajili

**Zungumza na daktari wako wa magojwa ya jumla (GP) au daktari kuhusu kujiandikisha katika MyMedicare, au upate maelezo zaidi kwenye health.gov.au/mymedicare**